TANGAZO LA SERIKALI Na. 10 La Tarehe 13/1/2023

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 107)*

NOTISI YA MSAMAHA WA KUSAFIRISHA NGUZO NA MAGOGO YA MKARATUSI MWEKUNDU NJE YA NCHI, 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Msamaha wa Kusafirisha Nguzo na Magogo ya Mkaratusi Mwekundu Nje ya Nchi ya Mwaka, 2023.

Msamaha wa kusafirisha nguzo na magogo

2.-(1) Kampuni ya Lutindi Legion Limited inapewa msamaha wa kusafirisha nguzo na magogo ya mkaratusi mwekundu yanayozidi kipenyo cha sentimenta ishirini kwenda nchini Ujerumani.

(2) Kiwango cha nguzo na magogo yaliyoruhusiwa kusafirishwa chini ya aya ndogo ya (1) kitakuwa kama kilivyoainishwa katika aya ya 4.

Sababu za msamaha

3. Sababu za kutolewa kwa msamaha huu ni-

(a) kampuni ya Lutindi Legion Limited imepata soko nchini Ujerumani la nguzo na magogo yanayozidi kipenyo cha sentimeta ishirini kinachoruhusiwa kisheria kusafirishwa nje ya nchi;
(b) msamaha huu utawezesha kupanua wigo wa huduma na biashara ya mazao ya misitu nje ya nchi; na
(c) kampuni ya Lutindi Legion Limited imeonyesha kwamba kuna usimamizi bora na matumizi endelevu ya nguzo na magogo ya mkaratusi mwekundu na kwamba soko

lililopatikana nje ya nchi litatoa mchango mkubwa katika uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu nchini.

Masharti ya msamaha

4. Msamaha huu unatolewa kwa masharti yafuatayo:

(a) idadi ya nguzo na magogo ya aina iliyotajwa katka Notisi hii hakitazidi elfu moja mia saba (1700) kama ifuatavyo-
   (i) nguzo *(Eukalyptus Red Round Poles)* mia moja (100) zenye ukubwa wa 30Cm x 30Cm x 8M;
   (ii) nguzo *(Eukalyptus Red Round Poles)* mia moja (100) zenye ukubwa wa 30Cm x 30Cm x 12M;
   (iii) magogo *(Eukalyptus Red)* mia tano (500) yenye ukubwa wa 30Cm x 30Cm x 15M;
   (iv) magogo *(Eukalyptus Red)* mia tano (500) yenye ukubwa wa 40Cm x 40Cm x 17M; na
   (v) magogo *(Eukalyptus Red)* mia tano (500) yenye ukubwa wa 44Cm x 44Cm x 19M;

(b) aina hii ya nguzo, magogo na kiwango tajwa itasafirishwa kwenda nchini Ujerumani.

Muda wa msamaha

5. Msamaha huu utatumika kwa kipindi cha siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Dodoma,
30 Desemba, 2022

PINDI H. CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*